Deaf Child Worldwide

# Viwango vya Chini katika Ulinzi na Usalama wa Watoto vya Deaf Child Worldwide

Deaf Child Worldwide

Viwango hivi vinatambuliwa kama mbinu bora zaidi na vinaweza kutumiwa na Deaf Child Worldwide, na mashirika yanayoshirikiana nasi, ili kutoa kigezo mahsusi ambacho ulinzi unaweza kupimwa na kutathminiwa.

Viwango hivi vinatoa mfumo kamilifu ambao washiriki wetu sharti watumie ili kufanya sera zao zifae mazingira na hali zao.

Pamoja na viwango hivi tunaandaa mafunzo ya mbinu za ulinzi wa watoto na maandalizi ya sera zinazowasaidia washiriki wetu.

# Kiwango cha 1: Sera

Shirika la Deaf Child Worldwide linapofanya makubaliano na taasisi shirikishi, linahitaji kwamba taasisi hiyo tayari iwe na sera, au iwe tayari kukuza sera ya ulinzi na usalama wa watoto. Sera hiyo sharti ifafanue mbinu ambazo zimewekwa ili kuzuia hatari kwa watoto na vijana wote na ifafanue jinsi ya kushughulikia kwa njia ifaayo masuala ya matatizo ya usalama yanayoweza kutokea.

## Kwa nini?

Kwa kuunda sera ya ulinzi na ya usalama wa watoto, taasisi zinaonyesha wazi kwamba zinaamini watoto sharti walindwe kila wakati na wasiwekwe katika hali ya hatari au unyanyasaji.

Sera lazima:

- izingatie kanuni za Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watoto (United Nations Convention of the Rights of the Child -UNCRC)
- ijumuishe maelezo sahihi ya ufafanuzi wa 'mtoto', 'kijana' na 'unyanyasaji' na kurejea aina tofauti za dhuluma na unyanyasaji.
- ijumlishe wafanyakazi wote, wafanyakazi wote wa kujitolea, wafanyakazi walio katika masomo, washauri, wakalimani wa lugha ya ishara na wageni katika miradi ya taasisi
- iidhinishwe na kukubaliwa na kamati ya uongozi husika ndani ya taasisi na kukaguliwa kila baada ya miaka mitatu
- ielezee wazi wazi majukumuya wasimamizi, wakurugenzi na wadhamini katika kuimarisha matumizi salama
- ijumuishe hatua zitakazofuatwa ikiwa wafanyakazi waandamizi na wadhamini wamedaiwa kukiuka sera.
- itangazwe ipasavyo, na kutafsiriwa katika lugha tofauti kutumia miundo tofauti ambayo inapatikana kwa watoto na vijana ambao ni viziwi na kusambazwa kwa wingi.

Hati zifuatazo zinaweza kutumiwa ili kutoa ushahidi kwamba vigezo vimetimizwa.

- Nakala ya sera, iliyotiwa sahihi na tarehe na usimamizi.
- Sera iliyotafsiriwa katika lugha za kienyeji.
- Mifano ya njia ambazo sera imesambazwa na kutangazwa, ikiwa ni pamoja na kwa watoto ambao ni viziwi na familia zao.

# Kiwango cha 2: Taratibu

Taasisi shirikishi sharti ziwe na au ziunde mazingira salama kwa watoto kwa kujumuisha michakato na taratibu za kuimarisha usalama wao katika mifumo yao iliyopo. Taratibu hizi sharti zifafanue kwa undani hatua zinazohitajika ili kutimiza sera ya ulinzi wa watoto na usalama wa watoto.

## Kwa nini?

Michakato na taratibu zifaazo za kuimarisha usalama wa watoto huhakikisha kwamba ulinzi wa watoto ni sehemu muhimu katika miundo yote ya shirika. Husaidia wafanyakazi kuwa na ujasiri wanaposhughulikia masuala au matatizo ya usalama yanayoweza kutokea. Hupunguza hatari katika miradi yote na katika taasisi.

Taasisi shirikishi sharti:

- ziendeleze taratibu zinazofaa mahali hususa za kuitikia na kuripoti matukio yanayogusia ulinzi wa watoto ambayo yanaweza kutokea ndani na nje ya taasisi yao.
- zijumuishe, katika sera zao, mwongozo kwa wafanyakazi wake kuhusu usiri, ulinzi wa data na jinsi ya kuhifadhi maelezo ya kibinafsi.
- zijumuishe katika sera yake, mwongozo wa matumizi ya picha, filamu na tafiti kuhusu watoto na vijana
- ziandae tararibu za kupata idhini kutoka kwa watoto na vijana ambao ni viziwi ili watumie picha na maelezo ya kibinafsi kuwahusu.

Hati zifuatazo zinaweza kutumiwa ili kutoa ushahidi kwamba kiwango hiki kimetimizwa.

- Chati zinazoripoti taratibu hatua kwa hatua ili kuonyesha wafanyakazi wanavyodhibiti na kusambaza maelezo ipasavyo kuhusu matukio na matatizo kuhusu ulinzi wa watoto.
- Mfano wa fomu za kutoa idhini zinazotumiwa na watoto au vijana ambao ni viziwi na wazazi wao.

# Kiwango cha 3: Watu

Mashirika yanayoshirikiana sharti yaweke wazi majukumu na matarajio ya wafanyakazi wake na wadau wake – na sharti yawaunge mkono ili kuelewa na kuendeleza shughuli kulingana na taratibu na sera ya ulinzi wa watoto na ya kuimarisha usalama wa watoto.

## Kwa nini?

Ulinzi wa watoto ni jukumu la kila mtu; kila mtu ana wajibu wakufanya. Mashirika yanahitaji kuhakikisha kuwa wale wote wanaohusika nao wanaelewa kuimarisha usalama wa watoto, hii ikijumuisha watoto na vijana viziwi na familia zao.

Mashirika yanayoshirikiana sharti:

- yateue wafanyakazi katika viwango tofauti vya shirika ambao wana jukumu la kuimarisha usalama, jukumu ambalo linafafanuliwa wazi kama sehemu ya kazi yao
- yahakikishe kwamba taratibu za kuwaajiri waajiriwa zimewekwa – taratibu hizi zinajumuisha kuwaajiri wafanyakazi wanaojitolea, wafanyakazi walio masomo na wakalimani wa lugha ya ishara
- yahakikishe wafanyakazi wote wamepewa mafunzo kamilifu kuhusu ulinzi wa watoto na kuimarisha usalama wa watoto na mafunzo yanatolewa upya kila mwaka na kuandaliwa upya baada ya kila miaka mitatu
- yahakikishe kuwa usimamizi wa wafanyakazi unazingatia ulinzi wa watoto na kuimarisha usalama wa watoto, kwa kutumia usimamizi, mikutano ya timu na tathmini ilikujadili masuala na matatizo yoyote yanayotokea
- yajumuishe Kanuni ya Maadili katika sera yao ya ulinzi wa watoto na kuimarisha usalama wa watoto, kanuni hii inafafanua jinsi wafanyakazi, wafanyakazi wanaojitolea, wafanyakazi walio masomo na wakalimani wanahitaji kujiendeleza
- yahakikishe kuwa wafanyakazi wote wanatia sahihi kwenye kauli ya kujitolea kulinda sera.
- yanakuza umuhimu wa ulinzi wa watoto na kuimarisha usalama wa watoto katika jamii na familia zao ambazo wanafanya kazi nazo.

Hati zifuatazo zinaweza kutumiwa ili kutoa ushahidi kwamba viwango vimetimizwa.

- Nakala ya mipango ya mafunzo na rekodi za mahudhurio ya kozi.
- Orodha ya anwani za wataalam, ushauri na maelezo ya wataalamu.
- Mifano ya matangazo ya kazi na mikataba ya uajiri, maombi na fomu ya kurejelewa.
- Kanuni za maadili mema.
- Miongozo ya taratibu za kuripoti za wafanyakazi, washirika, watoto na jamii.